Jarida la

Ligi Kuu

Septemba 2026

Uhuru Kuamua Nani Mbabe wa Kariakoo ‘DABI’ ya Ligi kuu ya NBC





SIMBA SPORTS CLUB 1936 VS YOUNG AFRICANS 1935 TANZANIA DAIMA MBELE NYUMA MWIKO

Oktoba 10

www.ligikuu.co.tz

KARIAKOO DERBY

NBC PREMIER LEAGUE

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

Hatua za kulipia King'amuzi cha Azam Tv kupitia **NBC Kiganjani App**

1. Fungua **NBC Kiganjani App**
2. Chagua Lipa Bili
3. Chagua TV
4. Chagua **Azam TV**
5. Weka namba ya king'amuzi
6. Weka kiasi au chagua kifurushi kinachotakiwa
7. Kamilisha malipo





Simba SC VS Young Africans

Jumamosi, Oktoba 10, 2026
Uhuru Stadium | Dar es Salaam
1:00 | Usiku

Yaliyomo

- Msimu wa Ligi 2026/2027.....2
- Pazia la Ligi Kuu ya NBC 2026/2027 lafunguliwa..... 4
- 'Wataalamu' 16 wanaosaka Taji la Ligi Kuu ya NBC 2026/2027.....5
- Nyota zao Zimeanza Kuonekana Asubuhi Ligi Kuu ya NBC.....7
- Vinara wa takwimu Ligi Kuu ya NBC 2026/2027.....9
- Jicho la Kiufundi.....11
- FVS yafungua enzi mpya ya Teknolojia soka la Tanzania.....14
- Wageni Kutoka Mali watembelea Tanzania Kujifunza.....16
- Hivi hapa viwanja vya Ligi Kuu 2026/2027.....17
- Ratiba ya NBC Championship, First League 'Yaanikwa' Kidigitali.....19
- NBC Championship 2026/2027 Kutimua Vumbi Septemba 11.....22
- Vita ya First League Kuanza Oktoba 21.....24
- Boli na Fasheni.....25







MAELEZO YA UCHAPAJI

Jarida hili huchapishwa kila mwezi na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania - TPLB

Mhariri Mkuu
Cornel Barnabas

Mhariri Habari
Yahaya Abushehe

Mhariri Msaidizi
Honest Mwanitega

Mpiga Picha
Loveness Bernard

Msanifu Kurasa
James Onesmo

Wachangiaji
Salma Seif
Pancras Remidius
Cynthia Michael
Sakina Abdoul
Collins Mwesigwa



Bodi ya Ligi Tuu Tanzania

Ghorofa na 14, NSSF Mafao House,
Barabara ya Uhuru - Ilala,
Dar es Salaam
S. L. P 79041 Dar es Salaam

www.ligikuu.co.tz
info@ligikuu.co.tz

Ligi Kuu

ligikuu | championshiptz | firstleague

tplboard

ligikuu

Ligikuu

LIGI KUU TV

NENO LA AFISA MTENDAJI MKUU

Mwezi Septemba umekuwa wa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, hususani katika kuhakikisha mashindano yanaendelea kwa ufanisi, kwa kuzingatia kanuni, viwango na taratibu zilizowekwa.

Baada ya kuanza kwa msimu mpya wa NBC Premier League mwezi Agosti, mwezi Septemba pia tulishuhudia kuanza rasmi kwa Ligi ya Championship ya NBC, hatua inayodhihirisha dhamira ya Bodi ya kuhakikisha mashindano yote yaliyo chini ya usimamizi wake yanaendeshwa kwa weledi na kwa viwango vinavyokubalika.

Msimu huu unaendelea kuja na matarajio makubwa kutoka kwa mashabiki, klabu, wadhamini, vyombo vya habari na wadau wengine wa soka. Kwa msingi huo, Bodi itaendelea kuweka mkazo katika ubora wa uendeshaji wa ligi, matumizi ya teknolojia, maendeleo ya miundombinu, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wadau.

Moja ya maeneo muhimu tunayoendeleza ni matumizi ya teknolojia katika kuboresha uendeshaji wa mashindano. Utekelezaji wa mifumo ya kidijitali katika maeneo mbalimbali, ikiwemo usimamizi wa taarifa, tiketi, Vibali vya kuingia uwanjani na shughuli nyingine za uendeshaji, ni sehemu ya mkakati wetu wa kujenga ligi yenye ufanisi, uwazi na inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia duniani.

Tunaendelea kukumbushana kuwa mafanikio ya ligi hayawezi kujengwa na Bodi pekee bali yanahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Bodi, klabu, wachezaji, makocha, waamuzi, wadhamini, vyombo vya habari, mashabiki na wadau wote wa mpira wa miguu.

Kwa mashabiki wetu, ambao ndiyo msingi mkubwa wa ukuaji wa ligi, tunawashukuru kwa kuendelea kuonesha upendo na kuunga mkono timu zenu. Tunawaomba kuendelea kuwa sehemu ya maendeleo ya soka letu kwa kuzingatia ustaarabu, kuheshimu wapinzani, viongozi wa mchezo na mali za umma. Ushabiki wenye heshima ndiyo unaojenga taswira nzuri ya soka letu. Tunapoendelea na msimu wa 2026/2027, nina imani kuwa kwa ushirikiano wa pamoja tutaweza kufikia malengo tuliyojiwekea na kuendelea kuongeza thamani ya mashindano yetu.

Bodi ya Ligi Kuu Tanzania itaendelea kuwa tayari kusikiliza, kujifunza na kuboresha.
Asanteni kwa kuendelea kuiamini na kuiunga mkono
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB).

Cornel Barnabas

Afisa Mtendaji Mkuu
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania





UHURU KUAMUA NANI MBABE WA KARIAKOO ‘DABI’ YA LIGI KUU YA NBC

SIMBA SPORTS CLUB 1936 VS YOUNG AFRICANS 1935 TANZANIA

Oktoba 10

DAR es Salaam inaingia katika wiki nyingine ya historia ya soka. Oktoba 10, 2026, macho ya Tanzania yataelekezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ambako Simba na Young Africans watakutana katika mchezo wa kwanza wa Kariakoo Derby wa Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/27.

Mchezo huo unaotarajiwa kuanza saa 1:00 usiku na hautakuwa pambano la kawaida la kupata alama tatu bali ni vita kati ya timu mbili ambazo zimeanza msimu kwa kasi zikishinda michezo yote sita ya kwanza na kukusanya jumla ya alama 18 kila mmoja huku tofauti ikiwa ni ya mabao pekee ambapo Young Africans imefunga mabao 16 na Simba imefunga mabao 11.

Kwa upande wa mabingwa watetezi timu ya Young Africans kinachovutia zaidi kwenye kikosi chao ni namna mabao yake yalivyogawanyika. Sio timu inayotegemea mfungaji mmoja pekee, Maxi Nzengeli raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo anaongoza kwa mabao matatu kwenye ligi, huku Mudathir Yahya, Albert Kangwanda na Peter Shalulile wakiwa na mabao mawili kila mmoja, Cheikh Ibrahima Touré, Chadrack Boka, Ibrahim Bacca, Mohamed Hussein na Farouk Koumara wamechangia bao moja kila mmoja kwenye kikosi hicho.

Kabla ya kuingia kwenye maandalizi ya moja kwa moja ya dabi, Yanga ilitumia mchezo wa kirafiki dhidi ya St George ya Ethiopia kama sehemu ya tathmini ya kikosi, na kushinda bao 1-0 kupitia bao la Albert Kangwanda.

Baada ya mapumziko mafupi, timu ilirejea mazoezini KMC Complex, lakini takribani wachezaji 15 walikuwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa na hilo limemlazimu Mngqithi kuanza maandalizi akiwa anasubiri kurejea kwa sehemu kubwa ya kikosi chake.

Kwa Taifa Stars, wachezaji wa Yanga waliokuwa kwenye majukumu ya kimataifa ni pamoja na Ibrahim Bacca, Bakari Mwamnyeto, Mohammed Hussein, Mudathir Yahya na Selemani Mwalimu. Kwa upande wa timu nyingine za taifa, Djigui Diarra alikuwa Mali, Housseine Zakouani Comoros, Albert Kangwanda Zambia, Peter Shalulile Namibia na Duke Abuya Kenya.

Hivyo, moja ya kazi kubwa ya Mngqithi katika siku chache zilizobaki ni kuhakikisha wachezaji wanaorejea kutoka safari tofauti wanaingia kwenye mfumo mmoja bila kupoteza kasi ambayo timu ilikuwa nayo kabla ya mapumziko.

Kama Yanga imechagua kuendelea na maandalizi yake Dar es Salaam, Simba imechukua njia tofauti ambapo ‘Wekundu wa Msimbazi’ walipeleka sehemu ya kikosi nchini Afrika Kusini kwa kambi ya takribani siku 10 katika mji wa Polokwane, chini ya kocha Steve Barker.

Lengo lilikuwa kupata muda wa kutosha wa kufanya kazi ya kimwili, kiufundi na kimfumo kabla ya kurudi Tanzania kwa ajili ya dabi. Simba ilipanga michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Polokwane City na Sekhukhune United kama sehemu ya tathmini hiyo.

Hata hivyo, matokeo ya michezo hiyo yameleta picha mbili tofauti ambapo Simba ilipoteza 1-0 dhidi ya Polokwane City, huku Barker akitumia mchezo huo kuwajaribu baadhi ya wachezaji katika nafasi ambazo si zao za kawaida.

Katika mchezo wa pili dhidi ya Sekhukhune United, Simba ilipoteza 2-1 hivyo, Simba imerejea Tanzania bila ushindi katika michezo hiyo miwili ya kirafiki, lakini thamani ya kambi hiyo kwa Barker haipimwi na matokeo pekee. Imetumika kumpa nafasi ya kuangalia muundo wa kikosi, wachezaji wanaoweza kubadilisha mfumo na wale wanaoweza kuingia kwenye kikosi cha kwanza.

Simba ilikuwa na wachezaji 10 waliokuwa kwenye majukumu mbalimbali ya timu za taifa, akiwemo Yusuph Kagoma, Morice Abraham na Nathaniel Chilambo waliokuwa Taifa Stars; Inno Loemba wa Congo Brazzaville na Djibrilla Kassali wa Niger, Pia kulikuwa na wachezaji waliokuwa kwenye timu za Tanzania U-23 na U-20.

Hii ina maana kwamba Barker alipata muda wa kufanya kazi na kundi moja Afrika Kusini, lakini sehemu nyingine ya kikosi ilikuwa kwenye majukumu ya kimataifa, kazi muhimu zaidi ni

kuunganisha makundi hayo mawili ya wale waliokuwa kambini Afrika Kusini na wale waliokuwa kwenye timu za taifa kuhakikisha wote wanaingia kwenye dabi wakiwa katika kiwango kinachofanana cha utayari wa kimwili na kiufundi.

Kwa upande wa takwimu za ufungaji, Simba ina mtu mmoja anayevutia zaidi kwenye mwanzo wa msimu ambaye ni Clatous Chama anayeongoza wafungaji wa Simba kwenye ligi akiwa na mabao manne. Ismael Olivier Touré na Rushine De Reuck wana mabao mawili kila mmoja, huku Anicet Oura, Libasse Gueye na Elie Mpanzu wakiwa wamechangia bao moja kila mmoja.

Kabla hata mpira haujapigwa Uhuru, tayari kuna ushindani mwingine unaoifanya dabi hii iwe tofauti, hii ni mara ya kwanza katika Ligi Kuu ya NBC msimu huu kwa Manqoba Mngqithi na Steve Barker kukutana kwenye dabi wakiwa makocha wa Yanga na Simba huku wote wakiwa raia wa Afrika Kusini.

Oktoba 10, saa 1:00 usiku, Uwanja wa Uhuru utakuwa kitovu cha macho ya soka la Tanzania, Simba ndiye mwenyeji wa mchezo huu, huku mchezo wa marudiano ukipangwa Februari 6, 2027 ambapo Yanga itakuwa mwenyeji, hii inaifanya dabi ya Oktoba 10 kuwa zaidi ya pambano la kwanza la ligi kati yao. Ni nafasi ya kwanza kwa kila upande kumshinda mpinzani wake moja kwa moja ndani ya mbio za ubingwa wa ligi baada ya wote kuanza kwa rekodi zinazofanana.

SIMBA MBABE WA ‘MZIZIMA’ LIGI KUU YA NBC.



Dabi ya Mzizima ni moja ya mchezo wenye hisia kwa wapenda soka na unaovutia mashabiki wengi wa Ligi Kuu ya NBC ambapo timu ya Azam ilikuwa mwenyeji wa timu ya Simba katika uwanja wa Azam Complex uliopo mkoani Dar es Salaam.

Kabla ya mchezo kuanza, hali ilikuwa ya presha kubwa, Simba iliingia uwanjani ikiwa na rekodi ya kushinda michezo yote mitano iliyokuwa imecheza ndani ya msimu wa 2026/2027 huku ikiwa na jumla ya alama 15.

Azam nayo ilikuwa imeshinda michezo minne, sare mbili huku ikikusanya alama 14 huku msimu uliopita timu ya Azam ilikusanya alama nne kutoka kwa Simba baada ya kushinda mchezo mmoja na kutoka sare mmoja.

Mchezo ulianza kwa kasi na timu zote mbili zilionekana kucheza kwa tahadhari, zikiheshimu uwezo wa wapinzani wao. Kipindi cha kwanza kilimalizika bila bao huku Simba ikiwa inaonekana kutawala mchezo na Azam wakionesha ari ya kuzitaka alama tatu muhimu.

Kipindi cha pili kilikuwa tofauti kabisa na timu ya Simba ilirejea uwanjani ikiwa na kasi na kuanza kushambulia zaidi katika eneo la timu ya Azam jambo lililowafanya Azam kupambana kuhakikisha wanajilinda.

Dakika ya 58 Simba ilipata bao la kwanza kupitia mpira wa kona uliopigwa na Nathaniel Chilambo na Rushine De Reuck alikwenda kuwania mpira huo ndani ya eneo la hatari hali iliyosababisha mkanganyiko mkubwa na beki wa kati wa Azam, Nathan Idumba alijifunga akijaribu kuokoa mpira huo.

Bao hilo lilibadilisha kabisa sura ya mchezo na timu ya Azam ililazimika kuongeza mashambulizi kwenye upande wa wapinzani wao huku ikitafuta bao la kusawazisha. Lakini kufanya hivyo kuliacha nafasi nyuma ya safu yake ya ulinzi jambo ambalo Simba ililitumia vizuri.

Dakika ya 67 Simba ilipata bao la pili baada ya kiungo wake Libasse Gueye kufanya kazi nzuri katikati ya uwanja na kuingia kwenye eneo la hatari kabla mpira haujampita na kumkuta Clatous Chama ambaye alitumia nafasi hiyo vizuri na kuongeza bao la pili kwa timu yake.

Bao hilo liliifanya Simba icheze kwa tahadhaari kubwa ikihakikisha inajilinda huku Azam nayo ikipambana kuhakikisha inapata chochote ndani ya mchezo huo na ilikuwa Simba ambayo ilimaliza kwa kuondoka na alama zote tatu’

Ushindi huo uliifanya Simba kufikisha alama 18 baada ya michezo sita na kuendeleza rekodi ya kutokufungwa mchezo wowote ndani ya msimu wa 2026/2027 huku Azam ikisalia na alama 14.

Dabi ya Mzizima ilionesha kuwa michezo mikubwa umiliki wa mpira pekee hauwezi kuamua matokeo bali mbinu zaidi za kiufundi za kocha Steven Barker na kutumia nafasi vizuri kuliifanya Simba kuibuka na ushindi.

Beki wa kati wa Simba, Rushine De Reuck alichaguliwa Mchezaji Bora wa mchezo huo kutokana na kiwango kizuri alichoonyesha katika mchezo huo.

HAWA HAPA WATAKAOAMUA ‘DABI’ YA KARIAKOO













Dabi ya Kariakoo ni moja ya michezo mikubwa barani Afrika huku ikitajwa kuwa ni dabi kubwa zaidi Afrika Mashariki na Kati ukiwa mchezo unaohusisha timu za Simba na Young Africans zenye maskani yake mitaa ya kariakoo mkoani Dar es Salaam.

Oktoba 10, 2026 timu ya Simba itakuwa mwenyeji wa timu ya Young Africa katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC katika mchezo utakaopigwa kwenye uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.

Ukubwa wa mchezo huo haufichiki ambapo macho na masikio ya wapenzi wa soka Tanzania, Afrika Mashariki, Bara la Afrika na Dunia kwa ujumla hufuatilia ‘miamba’ hiyo inapokutana kwani ni mchezo unaobeba historia kubwa ya soka la Tanzania.

Mara ya mwisho watani hao walipokutana kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya NBC walimaliza kwa sare ya mabao 2-2 kwenye uwanja wa Isamuhyo, Dar es Salaam na waliofunga mabao hayo kwa Simba walikuwa ni Libasse Gueye na Clatous Chama huku ya ‘wananchi’ yakifungwa na Prince Dube na nahodha Bakari Mwamnyeto.

Tukikaribia kushuhudia tena burudani hii kwa msimu huu kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu ya NBC, wafuatao ndio wana nafasi kubwa ya kuamua matokeo ya ‘mbungi’ hii ya Oktoba 10;

BARKER VS MNGQITHI

Steve Barker raia wa Afrika Kusini na Kocha Mkuu wa timu ya Simba ni tishio na mkali wa kucheza kwa mfumo mgumu wa kujilinda na kushambulkia kwa kasi akiwa anapendelea kutumia mfumo wa 4-2-3-1 na 4-3-3 ambapo hadi sasa timu yake haijapoteza mchezo wowote ndani ya Ligi Kuu ya NBC huku ikiwa ni msimu wake wa pili ndani ya ligi hiyo na dabi zote walitoka sare ya 0-0 na 2-2.

Manqoba Mngqithi ni raia wa Afrika Kusini pia na Kocha Mkuu wa klabu ya Young Africans akiwa katika msimu wake wa kwanza ndani ya Ligi Kuu ya NBC akiwa ameiongoza klabu yake hadi sasa kwenye michezo sita na kushinda yote. Anapenda kutumia zaidi mfumo wa 4-3-3 huku akipendelea kuwasoma wapinzani wake na mara nyingi anapendelea timu yake kushambulia kwa kasi na kufunga mabao mengi zaidi, ndio maana timu yake imefunga mabao 16 ndani ya michezo sita na kuwa kinara wa mabao hadi sasa kwenye Ligi Kuu ya NBC.

DIARRA VS KASSALI

Hakuna asiyefahamu ubora wa magolikipa wa timu zote mbili Djigui Diarra wa Young Africans aliyefanikiwa kukusanya ‘cleansheet’ nne ndani ya michezo sita sawa na Mahamadou Kassali wa Simba mwenye cleansheet nne ambapo ulinzi wao wa kutokuruhusu mabao ndio unaonekana kuwa chachu ya kuamua ni timu ipi ibebe alama tatu ndani ya mchezo huo wa wababe hao wa Kariakoo.

GUEYE vs NZENGELI

Libasse Gueye kiungo wa timu ya Simba amefanikiwa kuhusika kwenya mabao sita msimu huu akifunga bao moja na pasi saidizi za mabao tano. Aidha mchezaji huyo amefanikiwa kuwa mchezaji bora wa mwezi agosti wa Ligi Kuu ya NBC huku ubora wake ndani ya kikosi cha Simba hakuna anayeweza kutilia mashaka hivyo ni mmoja wa wachezaji wa kuangaliwa sana kwenye mchezo wa Kariakoo dabi kwani anaweza kuamua matokeo muda wowote.

Kwa upande wa Maxi Nzengeli ni kiungo wa klabu ya Young Africans aliyefanikiwa kuhusika katika mabao Matano akifunga mabao matatu na kutoa pasi saidizi mbili huku akifanikiwa kuchaguliwa kuwa mchezaji bora katika michezo mitano kati ya sita ambayo timu hiyo imecheza hadi sasa na ubora wake unaweza kuamua mchezo wa dabi ya oktoba 10.

CHAMA vs KANGWANDA

Clatous Chama ni mchezaji wa Simba aliyecheza dabi nyingi zaidi ndani ya kikosi hicho akiwa amefanikiwa kufunga mabao manne ndani ya msimu huu wa 2026/2027 wa Ligi Kuu ya NBC. Mchezaji huyo ni mmoja wa wachezaji waliofunga bao dabi iliyopita ambayo iliisha kwa 2-2 na ubora wake kwenye eneo la ushambuliaji na utulivu wake unaweza kuibeba timu hiyo katika mchezo dhidi ya watani wao.

Kwa upande wa Albert Kangwanda ni mshambuliaji wa Young Africans ambaye ndani ya msimu wa 2026/2027 amefanikiwa kufunga mabao mawili na kutoa pasi za mabao mbili, akihusika katika mabao manne kati ya mabao 16 ambayo timu hiyo imeweza kufunga na ubora wake utaweza kusaidia timu katika kukimbia na namna anavyotumia nafasi akipata mpira.

SHALULILE vs MPANZU

Peter Shalulile mshambuliaji wa Young Africans hii itakuwa dabi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ya NBC ndani ya msimu huu akiwa amesajiliwa na timu hiyo kutoka Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini amefanikiwa kufunga mabao matatu hadi sasa. Ubora wake katika kumalizia mipira, namna anavyoweza kukimbia anapokuwa na mpira na anavyoweza kutafuta mpira ataweza kuisaidia timu yake kupata ushindi katika mchezo huo.

Ellie Mpanzu mchezaji wa klabu ya Simba anaweza kucheza nafasi nyingi kama vile winga zote mbili na hata kuwa mshambuliaji kivuli (False9). Ndani ya msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC ameweza kuisaidia timu yake kwa kufunga bao moja na kutengeneza mikimbio iliyowapa nafasi wachezaji wenzake kufunga na kuisaidia timu hiyo. Ingawa amefunga bao moja pekee hadi sasa lakini ubora wake anapokuwa uwanjani sio kitu cha kubezwa hivyo timu ya Young Africans inapaswa kuwa makini na winga huyu kwani anaweza kuamua mchezo wakati wowote.

TOURE VS BACCA

Ismael Toure beki wa kati wa Simba ni mzuri sana katika kufunga mabao ya kichwa na ameipatia timu yake mabao mawili huku uwezo wake wa kukaba ukifanya timu yake kuwa salama muda mwingi. Anaisaidia timu yake kuwa na namba kubwa wakati wa kupiga mipira ya kona na mipira ya kutenga kutokana na faida ya kimo chake hivyo atakuwa mmoja wa wachezaji wa kuchungwa zaidi ndani ya mchezo wa Dabi.

Ibrahim Hamadi (Bacca) ni beki wa kati wa timu ya Young Africans, ni mzuri sana katika kucheza mipira ya chini na pia kufunga mabao ya kichwa, akiipatia bao moja timu yake na pia anahusika katika kuimarisha ulinzi katika lango lao ambalo limeruhusu mabao mawili pekee hadi sasa msimu huu jambo linalowafanya wapinzani kujipanga zaidi wanapotaka kucheza na timu hiyo na hivyo dabi itakuwa ya pekee kutokana na uwepo wake.

ZAKOUANI vs OURA

Housseine Zakouani ni kiungo mshambuliaji wa Young Africans ambaye hadi sasa ametoa pasi tatu za usaidizi wa mabao akiwa na uwezo wa kupiga chenga na jicho lake la kuona wachezaji wenzie wanaokuwa kwenye nafasi na kuwapasia hivyo atakuwa mchezaji wa kuchungwa katika dabi hii kutokana na kasi yake awapo uwanjani.

Anicet Oura ni kiungo mshambuliaji wa Simba ambae ana kasi, akili na nguvu ya kukokota mpira akiwa amesaidia timu yake kwa kufunga bao moja na kutoa pasi moja ya usaidizi hadi sasa kwenye Ligi Kuu ya NBC, kimo chake na uwezo wake wa kufunga mabao ya kichwa ni tishio na wa kuchungwa kuelekea dabi hii.

BOKA VS CHILAMBO

Chadrack Boka beki wa kushoto wa Young Africans ana sifa ya kasi ya ajabu awapo ndani ya kiwanja, ameisaidia timu yake hadi sasa kwa kufunga mabao mawili na kutoa pasi za usaidizi mbili ni tishio kwa mabeki wavivu kiwanjani na mchezaji wa kutumainiwa kwa klabu yake, mchango wake mkubwa ni kuwepo katika maeneo yote ya uwanja kwa kulinda na kushambulia.

Nathaniel Chilambo ni beki wa kulia wa timu ya Simba ambaye ana uwezo wa kucheza nafasi zaidi ya moja awapo ndani ya kiwanja. Akiwa ametoa pasi saidizi moja hadi sasa na anapokuwa kiwanjani anaipa timu yake faida ya kulinda wakiwa hawana mpira na faida ya kuongezeka kama kiungo wanapokuwa wanashambulia na uwezo wa kuwapunguza mabeki akiongezeka kwenye safu ya kiungo. Huyu hana tofauti sana na Chadrack Boka na ikiwa wote watapata nafasi ya kuanza katika mchezo huo basi upande wao utakuwa na 'amsha amsha' nyingi kutokana na uwezo wao wa kucheza mpira.





TASWIRA YA MWANZO WA LIGI KUU YA NBC.

POS	TEAM	P	W	D	L	GF	GA	GD	PTS
1	Young Africans SC	6	6	0	0	16	2	14	18
2	Simba SC	6	6	0	0	11	2	9	18
3	Azam FC	7	4	2	1	11	7	4	14
4	Singida Black Stars	6	3	1	2	13	9	4	10
5	Polisi Tanzania	6	3	1	2	9	7	2	10
6	Mbeya City	6	3	1	2	6	4	2	10
7	Dodoma Jiji	6	3	1	2	4	4	0	10
8	Mashujaa FC	6	3	0	3	6	6	0	9
9	Geita Gold	6	2	1	3	9	8	1	7
10	JKT Tanzania	6	2	1	3	7	10	-3	7
11	Coastal Union	6	2	1	3	6	9	-3	7
12	TRA United SC	6	1	3	2	6	6	0	6
13	Namungo FC	7	2	0	5	6	11	-5	6
14	Fountain Gate	6	1	1	4	2	9	-7	4
15	Kagera Sugar	6	0	2	4	5	14	-9	2
16	Pamba Jiji FC	6	0	1	5	4	13	-9	1

LIGI Kuu ya NBC imeendelea kushika kasi kwenye viwanja mbali mbali huku kila timu ikijaribu kupambania alama muhimu mwanzoni ili kujiweka salama mwisho wa msimu. Hadi sasa ni timu mbili pekee za Young Africans na Simba zimepata ushindi wa asilimia 100 huku zikitarajiwa kukutana Oktoba 10 kwenye mchezo wa Kariakoo 'dabi'.

Young Africans ndiye kinara wa Ligi Kuu ya NBC akiwa amecheza michezo sita na kushinda yote, akikusanya alama 18 na kufunga jumla ya mabao16 huku akiwa ameruhusu mabao mawili na kupata ushindi kwa asilimia 100%.

Timu ya Simba inashika nafasi ya pili ikiwa imecheza michezo sita na kupata ushindi katika michezo yote pia kama Young Africans huku ikiwa imefanikiwa kukusanya alama 18 kwa kufunga ya mabao 11 na kuruhusu kufungwa mabao mawili ikiwa ni sawa na ushindi wa asilimia 100% na 'mnyama' akizidiwa na mtani wake kwa tofauti ya mabao.

Azam ipo nafasi ya tatu na alama 14, ikicheza michezo saba na kupata ushindi mara nne, kupoteza mara moja dhidi ya Simba kwenye uwanja wake wa nyumbani na sare mbili, ikifanikiwa kufunga mabao 11 na kuruhusu mabao saba sawa na ushindi wa asilimia 57%.

Singida Black Stars ipo nafasi ya nne ikiwa na alama 10 katika michezo sita iliyocheza mpaka sasa, huku ikiwa imefanikiwa kufunga mabao 13 pamoja na kuruhusu mabao tisa, aidha timu hiyo imepata sare moja, kupoteza michezo miwili na kushinda michezo mitatu sawa na ushindi wa asilimia 50%.

Polisi Tanzania iliyopanda Ligi Kuu ya NBC msimu huu baada ya kuitoa Tanzania Prisons kwenye mchezo wa mtoano inashika nafasi ya tano ikiwa imecheza michezo sita na kukusanya jumla ya alama 10 kwa kupata ushindi mara tatu, sare moja na kupoteza michezo miwili huku wakifunga jumla ya mabao tisa na kuruhusu mabao saba, ushindi wao ukiwa ni wa asilimia 50%.

Mbeya City inashika nafasi ya sita ikiwa imecheza mechi sita na kupata jumla ya alama 10. Timu hiyo imefunga jumla ya mabao sita na kuruhusu mabao manne, aidha Mbeya City imeshinda michezo mitatu sare moja na kupoteza mara mbili sawa na ushindi wa asilimia 50%.

Dodoma Jiji inashika nafasi ya saba ikiwa imecheza michezo sita na kukusanya jumla ya alama 10 huku ikifanikiwa kufunga mabao manne na kuruhusu mabao manne, aidha imeshinda michezo mitatu, kupoteza michezo mitatu na sare moja ikiwa ni sawa na ushindi wa asilimia 50%.

Mashujaa wanashika nafasi ya nane huku wakiwa wamecheza michezo sita na kuvuna alama tisa, wamefunga mabao sita na kufungwa sita, timu hiyo imeshinda michezo mitatu, kufungwa michezo mitatu sawa na ushindi wa asilimia 50%.

Geita Gold inashika nafasi ya tisa ikiwa imecheza michezo sita na kuvuna alama saba, imefanikiwa kufunga mabao tisa na kuruhusu mabao nane, imeshinda michezo miwili, sare moja na kupoteza michezo mitatu sawa na asilimia 33%

JKT Tanzania inashika nafasi ya 10 ikiwa imecheza michezo sita na imefanikiwa kuvuna jumla ya alama saba, kushinda michezo miwili sare moja na kupoteza michezo mitatu, ikiwa imefunga mabao saba, kuruhusu kufungwa mabao 10 na kupata ushindi wa asilimia 33%

Coastal Union inashika nafasi ya 11 ikiwa imecheza jumla ya michezo sita, ikikusanya alama saba huku ikiwa imefunga jumla ya mabao sita, kuruhusu mabao tisa, imeshinda michezo miwili sare moja na

kupoteza mara tatu sawa na ushindi wa asilimia 33%.

TRA united wanashika nafasi ya 12 ikiwa imecheza michezo sita na kukusanya jumla ya alama sita, imefunga mabao sita na kufungwa mabao sita aidha imeshinda mchezo mmoja, kupoteza michezo miwili na sare tatu sawa na asilimia 17% za ushindi.

Namungo inashika nafasi ya 13 ikiwa imecheza michezo saba na kukusanya jumla ya alama sita, ikiwa imefunga mabao sita na kuruhusu mabao 11 huku timu hiyo ikishinda michezo miwili na kupoteza mara tano sawa na asilimia 29% za ushindi.

Fountain Gate inashika nafasi ya 14 ikicheza michezo sita na kukusanya alama nne, imeshinda mchezo mmoja sare moja na kupoteza michezo minne huku timu hiyo ikifanikiwa kufunga mabao mawili na kuruhusu mabao tisa sawa na ushindi wa asilimia 17%.

Kagera Sugar inashika nafasi ya 15 ikiwa imecheza michezo sita na kukusanya alama mbili zilizotokana na sare mbili na ikipoteza michezo mine, imefanikiwa kufunga mabao matano na kuruhusu mabao 14 sawa na ushindi wa asilimia 0%.

Pamba Jiji inashika nafasi ya 16 na ya mwisho ikiwa imecheza jumla ya michezo sita na kupata alama moja. Haijapata ushindi katika mchezo wowote, imepata sare moja ambayo ilikuwa dhidi ya Dodoma Jiji kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya NBC msimu huu na kupoteza michezo mitano. Aidha timu hiyo imefunga jumla ya mabao manne na kuruhusu mabao 13 ikiwa na asilimia 0% za ushindi sawa na majirani zao wa Kanda ya ziwa timu ya Kagera Sugar.







Jicho la Kiufundi

Na **Sisti Martin** sistinho

LIGI KUU SEPTEMBA ULIKUWA MWEZI WA ‘SET PIECES’

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya magoli yanayofungwa kwenye mpira wa miguu hutokana na mipira ya kutenga (Set Plays/Pieces) kama Kona (Coerner Kicks), Mapigo huru (Freekicks), Penalti (Penalty Kicks) na mipira ya kurusha hali inayofanya nyakati za mipira ya kutenga kuwa moja ya nyakati za muhimu za kimbinu na zinazohitaji umakini mkubwa kwa timu kuzuia au kushambulia.

Kati ya jumla ya magoli 30 yaliyofungwa kwenye mechi 13 za Mwezi Septemba 2026 kwenye Ligi kuu ya NBC, magoli 14 yametokana na mipira ya kutenga sawa na asilimia 46 ya magoli hayo na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo;

(i) Magoli yaliyotokana na Kona – 6
(ii) Magoli yaliyotokana na Freekicks – 4
(iv) Magoli yaliyotokana na Penalti – 4

KONA (Corner Kicks)

Kati ya magoli 30 yaliyofungwa kwa mwezi Septemba, magoli 6 yametokana na kona huku kukiwa na ubora na udhaifu kwa pande za timu zote 2 zinazozuia na kushambulia kona hizo.

Kati ya magoli hayo 6 ya kona, magoli matatu yametokana na kona za kupigwa moja kwa moja huku wachezaji wakishinda mipira ya juu (Aerial Duels) na kufunga ambapo Magoli hayo ni Goli la kwanza la Polisi Tanzania dhidi ya Mbeya City lililofungwa na Anuary Jabir kona ikipigwa na Denis Mushi, Goli la kwanza la Mashujaa FC dhidi ya Singida BS lililofungwa na Samson Madeleke, Goli la pekee la Yanga dhidi ya Geita Gold lililofungwa na Comara kona ikipigwa na Max Nzengeli

Magoli mengine mawili ya kona yametokana na kushindania mipira kugombania baada ya mpira wa juu (50/50 or Second balls) nayo ni kama ifuatavyo; Goli la kwanza la Coastal Union dhidi ya Polisi Tanzania lililofungwa na Maabad Maabad aliyeshinda mpira wa kugombania wanne baada ya mpira wa kwanza wa kona, Goli la pekee la Kagera Sugar dhidi ya Fountain Gate lililofingwa na Masanja baada ya Kambenga kushinda mpira wa kona uliopigwa na Saleh.

Goli moja la Kona lililobaki limetokana na mpira wa kujifunga, nalo ni goli la kwanza la Simba SC dhidi ya Azam FC baada ya beki wa Azam FC kujifunga mpira wa kona uliopigwa na Nathanael Chilambo.

MAPIGO HURU (Freekick)
Kati ya magoli 30 yaliyofungwa kwa mwezi Septemba, magoli 4 yametokana na mapigo huru/ Freekicks huku kukiwa na udhaifu na ubora kwa pande zote 2 zinazozuia na kushambulia mapigo hayo.

Kati ya magoli hayo manne ya Freekick, magoli mawili yametokana na mipira ya Freekick za moja kwa moja zilizopigwa na kulenga lango ambayo ni Goli la pekee la Pamba Jiji dhidi ya TRA United lililofungwa na Abdulkarim Yunus baada ya John Nakibinge kuchezewa madhambi na Goli la pekee la JKT Tanzania dhidi ya Coastal Union lililofungwa na Otaro.

Kati ya magoli hayo manne ya Freekick, magoli mawili mengine yametokana Freekick zisizo za moja kwa moja hasa kushindania mipira kugombania ya juu na mipira ya pili (Aerial Duels or Second balls) kama ifuatavyo; Goli la kwanza la Dodoma Jiji dhidi ya Mashujaa lililofungwa na Beno Ngassa aliyeshinda mpira wa chini baada ya mipira kadhaa ya kugombania, Goli la pili la Mashujaa dhidi ya Singida BS lillofungwa na Lyawatwa baada ya mpira wa pili uliodondoka baada ya Ngushi kushinda mpira wa juu.

MIKWAJU YA PENALTI (Penalty Kicks)
Magoli manne kati ya 30 yaliyofungwa kwa mwezi huo yametokana na mipira ya adhabu za mikwaju ya Penalti iliyotokana na adhabu mbalimbali.

Mkwaju mmoja wa penalti umetokana na mchezaji wa Polisi Tanzania kuunawa mpira kwenye eneo la hatari na kuisababishia timu yake kupata adhabu ya mkwaju wa Penalti uliopigwa na Maabad Maabad.

Mikwaju mitatu ya penalti imetokana na wachezaji wa timu zinazoshambulia kuchezewa isivyofaa kwenye eneo la hatari na timu zao kufaidika na mkwaju wa Penalti ambayo ni Goli la pili la Namungo FC dhidi ya Singida BS lililofungwa na Rogers Gabriel baada ya kuchezewa isivyofaa na Imoro Ibrahim, Goli la pili la Polisi Tanzania dhidi ya Mbeya City lililofungwa na Anuary Jabir, Goli la kwanza la Coastal Union dhidi ya JKT Tanzania lilofungwa na Maabad Maabad baada ya mchezaji wa Coastal Union kuchezewa isivyofaa na kipa wa JKT Tanzania, Ramadhan Chalamanda

HITIMISHO
Kwenye magoli yote yanayotokana na mipira ya kutenga, mapungufu na ubora yamekuwa yakihusu zaidi wachezaji hasa utayari wa kuweza kushinda mipira ya juu na inayodondoka, ni mara chache sana mbinu za makocha huwa na athari chanya na hasi, mara nyingi athari zao hujitokeza kwa wachezaji kujua au kutojua maeneo wanayopaswa kuwepo kwa nyakati sahihi ili kuepuka kufanya makossa yanayoweza kuzaa magoli au adhabu zaidi.





NBC CHAMPIONSHIP 2026/27 KUTIMUA VUMBI SEPTEMBA 11

Msimu wa 2026/2027 wa Ligi ya Championship ya NBC umeanza rasmi Septemba 11 huku ukizihusisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Timu hizo ni Rhino Rangers na Mbeya Kwanza kutoka mkoa wa Tabora, Tanzania Prisons na KenGold kutoka mkoa wa Mbeya, KMC, Kigamboni United na Transit Camp kutoka mkoa wa Dar es Salaam, IAA na Mbuni kutoka mkoani Arusha, TMA ya mkoani Iringa, Mtibwa ya Morogoro, Bandari ya Mtwara, Gunners ya Dodoma, Songea United ya mkoani Ruvuma na Bigman ya Tanga.

Mzunguko wa kwanza wa Ligi hiyo ulihusisha michezo minane ambayo ilionyesha namna ambavyo timu hizo zinapambana kusaka alama za kupanda daraja kwenda Ligi Kuu ya NBC msimu ujao.

Michezo ya ufunguzi ilichezwa katika viwanja vitatu ambapo KMC iliikaribisha timu ya Mbuni katika uwanja wa KMC Complex mkoani Dar es Salaam, Rhino Rangers ikiwa mwenyeji wa timu ya Tanzania Prisons katika uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora na Kigamboni United ikialika timu ya TMA katika uwanja wa Uhuru Dar es Salaam.

Ilichukua dakika tisa tu mchezaji wa KMC, Ramadhan Kalanje kufungua msimu huo kwa bao la kwanza la Ligi ya Championship ya NBC katika mchezo wa KMC dhidi ya Mbuni na mchezo huo uliisha kwa matokeo ya 5-1.

Rhino Rangers aliibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons bao lililofungwa na Zuberi Malila huku timu ya Kigamboni United ikiwaliza TMA kwa 1-0 bao lililofungwa na Nicodemus Ntarema ikiwa michezo hiyo ilichezwa majiira ya saa kumi jioni.

Septemba 12, KenGold iliikaribisha timu ya Bandari katika uwanja wa Manispaa ya Chunya na timu ya KenGold ambapo walitoka sare ya 1-1 na Stand United ya mkoani Shinyanga ikiichapa Mbeya Kwanza 2-1 mchezo uliochezwa uwanja wa Kambarage Shinyanga.

Septemba 13, timu ya IAA ilicheza na Bigman katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid na kufanikiwa kuifunga Bigman 2-1, Songea United ilicheza na Gunners katika uwanja wa Majimaji Ruvuma na matokeo yalikuwa sare 1-1.

Septemba 14, Transit Camp ilicheza na Mtibwa Sugar katika uwanja wa KMC Complex na matokeo ilikuwa sare ya 1-1.

KMC ndio timu iliyofunga mabao mengi zaidi ndani ya mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ikiwa ni matano huku michezo mitatu kati ya minane iliisha kwa sare, wakati timu tano zilianza msimu kwa ushindi na kupata alama tatu katika mchezo wao wa kwanza.

Mwanzo huo unaweka msingi wa msimu wenye ushindani huku kila timu ikiendelea kutafuta alama muhimu katika safari ya Championship 2026/2027 na kupambania nafasi ya kupanda daraja moja kwa moja ama walau kucheza hatua ya mtoano.



‘BOLI’ & ‘FASHENI’

Nathanael Chilambo

Juma Mgunda

TUNAKUONA MBALI

FAMILIA

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

Nunua tiketi ya **Qatar Airways**
na **NBC Visa Card** upate

PUNGUZO LA 12%



#NBCVisaCard

VISA | QATAR AIRWAYS القطرية